FEED THE FUTURE
The U.S. Government's Global Hunger & Food Security Initiative

OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA

TARATIBU ZA KULIPA USHURU WA MAZAO MCHANGANYIKO, MAZAO YA MALIASILI NA MAZAO MCHANGANYIKO YANAYOSAFIRISHWA NCHI ZA NJE

Kwa kuzingatia Sheria Ndogo (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Kyela za Mwaka 2018, Kifungu cha 4.

UTANGULIZI

Maana ya ushuru wa mazao; ni ada inayotozwa na Halmashauri kwenye mazao.

Ushuru wa mazao unatozwa kwenye mazao ya aina tatu:

i. Mazao mchanganyiko;Mahindi, maharage, mpunga, mchele, muhogo, matunda, mawese, mazao mengine na kakao.
ii. Mazao ya maliasili; Mbao, gogo kubwa, gogo la kati, gogo dogo, mkaa na kuni.
iii. Mazao yanayosafirishwa nnje ya nnchi; Mahindi, maharage, mpunga, mchele, muhogo, matunda, mawese na mazao mengine.

Lengo; Kuongeza mapato ya Halmashauri ili kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo

Faida za kulipa ushuru wa mazao:

- **Kwa Halmashauri**
  - 20% ya makusanyo ya mapato kutumiaka kuendeleza sekta ya kilimo wilayani
  - 60% ya makusanyo yanayobaki hutumika katika kukamilisha miradi mbalimbali ya Halmashauri kulingana na bajeti ya mwaka husika ikiwemo kuimarisha miradi inayoibuliwa na wananchi

- **Kwa Mfanyabiashara/Kampuni**
  - Kufanya biashara kwa uhuru bila kubugudhiwa
  - kufaidika na miradi ya serikali kama ujenzi wa barabara, usafi wa mazingira n.k
  - Kuwa na usalama wa mizigo wakati wa usafirishaji mfano kama kutatokea wizi risiti ya ushuru itaonyesha uhalali wa mizigo ya mfanya biashara/kampuni

Mamlaka zinazohusika na ukusanyaji wa ushuru wa mazao - Halmashauri ya wilaya ya Kyela kupitia watendaji wa kata, watendaji wa vijiji na mawakala mbalimbali wenye mikataba na Halmashauri.

Wanaowajibika kulipa ushuru wa mazao:
- Wafanyabiashara wa mazao yote yanayolimwa ndani na nje ya wilaya
- Wafanyabiashara mwenye uhalali wa kufanya biashara ya mazao ndani ya wilaya
- Wajasiriamali wadodo wadogo wa biashara za mazao

Tozo anazotozwa mfanyabiashara ni pamoja na:
- Ada ya maombi ya kibali cha ununuzi wa mazao Tshs. 20,000/=
- Ada ya kibali cha ununuzi kwa mwaka wa fedha husika Tshs. 300,000/=
- Ada ya ushuru wa huduma kulingana na makadirio ya kiasi cha mzigo atakaonunua kwa mwaka mzima

Mfanyabiashara akishalipa tozo hizi anatakiwa aende wilayani kwajili ya kupata kibali cha kununua mazao na kisha kulipia ushuru kama inavyoelekezwa (rejea jedwali lililoambatanishwa kwaajili ya ada husika)

TARATIBU ZA KULIPA USHURU

Mnunuzi afanye yafuatayo:

i. Aandae kituo cha kukusanyia mazao
ii. Apate kibali cha ununuzi wa mazao kutoka wilayani
iii. Alipe ushuru wa mazao katika eneo (Kijiji/Kata) husika anaponunulia mazao

USAID FROM THE AMERICAN PEOPLE

iesc

OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA

Mambo muhimu:

- Mazao yote ndani ya Halmashauri yatauzwa katika maeneo maalum yaliyotengwa na Halmashauri kwa shughuli hiyo, na kwa mujibu wa Jedwali la 17 la Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Kyela ya mwaka 2018, chini ya kifungu cha 4.
    - Masoko ya samaki na dagaa ni mwalo wa; Ikombe, Ikubo, Muungano, Lugombo, Matema, Rubaga, Kapugi na Njisi/Kafyofyo.
- Mazao yote yatapimwa kwa ujazo wa kilo na kila gunia litahesabiwa kwa kilo Mia moja (100) au kipimo kingine kitakachokubaliwa na Halmashauri.
- Muda wa kusafirisha Mazao au bidhaa yoyote inayotakiwa kulipiwa ushuru kwa Halmashauri itakuwa kuanzia saa 12.30 Asubuhi hadi saa 12.30 jioni, isipokuwa mazao yanayoharibika haraka ambapo yataruhusiwa kusafirishwa kwa kibali maalum.

TARATIBU ZA KUSIMAMIA UTEKELEZAJI NA MOTISHA

Taratibu za kusimamia utekelezaji

Na.	KOSA	ADHABU	
1	Ununuzi wa mazao bila ya kuwa na vibali	Faini isiyopungua shilingi laki mbili (200,000/=) na isiyozidi shilingi milioni moja (1,000,000/=) Au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne (24) Au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo	Pamoja na; kulipia kibali cha ununuzi kabla ya kuachiwa na kuendelea na shughuli zake.
2	Mfanyabiashara mwenye kibali kukwepa ushuru		Pamoja na; kupewa onyo, akirudia kosa anaweza kunyang'anywa kibali cha ununuzi wa mazao
3	Kusafirisha mazao nje ya Wilaya baada ya muda ulioruhusiwa ambao ni; kuanzia saa 12.30 asubuhi hadi saa 12.30 jioni, isipokuwa mazao yanayoharibika haraka ambapo yataruhusiwa kusafirishwa kwa kibali maalum.		Pamoja na; kuzuiwa kuendelea na safari hadi siku inayofuata

Motisha na/au Msamaha

- Wakulima wanaosafirisha mazao yao kutoka mashambani chini ya tani moja (1), hawalipi ushuru wakiwa na vibali vya uthibitisho wa mahali alipolima mazao kutoka kwa serikali ya kijiji husika
- Wajasiriamali wenye vitambulisho vya ujasiriamali wenye mitaji chini ya Tshs. 4,000,000/= hawatozwi ushuru (Agizo la Rais, 2018)

FEED THE FUTURE
The U.S. Government's Global Hunger & Food Security Initiative

OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA

USHURU WA MAZAO MCHANGANYIKO, MAZAO YA MALIASILI NA MAZAO MCHANGANYIKO YANAYOSAFIRISHWA NCHI ZA NJE

1. **Ushuru wa Mazao Mchanganyiko**

Na.	ZAO	KIWANGO
1	Mahindi	3% ya bei ya kununulia kwa gunia la kilo 100
2	Maharage	
3	Mpunga	
4	Mchele	
5	Muhogo	
6	Matunda	
7	Mazao mengine	
8	Kakao	
9	Mawese	3% kwa lita 20

2. **Ushuru wa Mazao ya Maliasili**

Na.	AINA YA MALIASILI	KIWANGO
1	Mbao	Tsh. 150/= kwa kila ubao
2	Gogo kubwa	Tsh. 5,000/= kwa kila gogo
3	Gogo la kati	Tsh. 3,000/= kwa kila gogo
4	Gogo dogo	Tsh. 2,000/= kwa kila gogo
5	Mkaa	Tsh. 2,000/= kwa kila gunia
6	Kuni	Tsh. 5,000/= kwa tani moja

3. **Ushuru wa Mazao Mchanganyiko Yanayosafirishwa Nchi za Nnje**

Na.	ZAO	USHURU
1	Mahindi	10% ya bei ya kununulia kwa gunia la kilo 100
2	Maharage	
3	Mpunga	
4	Mchele	
5	Muhogo	
6	Matunda	
7	Mawese	
8	Mazao mengine	

Ushuru unaweza kuchajiwa chini ya asilimia/kiwango kilichotajwa hapo juu kwa kuzingatia maoni ya timu ya wataalamu wa wilaya wakati wa maandalizi ya bajeti na wadau wa zao husika.